n) Tumia nomino dhahania kutokana na kitenzi 'weza' kutunga sentensi. (alama 2)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

o) Tunga sentensi tatu tofauti ukitumia neno : kote , kama – kivumishi, kielezi na kiwakilishi. (alama 3)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

p) Tambua vihusishi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

Vibarua walilima kutoka hapa.

Wote waliahidi kujaribu kulingana na nguvu zao.

........................................................................................................................................

q) Eleza maana mbili za sentensi hii (al.2)

Simon anampenda Jane kuliko uimbaji

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

r) Tunga sentensi kubainisha dhana ya kuamrisha ukitumia kitenzi soma katika umoja na wingi (alama 2)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

**D: ISIMU JAMII** (al. 10)

a) Fafanua dhana hizi za isimu jamii. (alama 5)

i) Jamii- lugha ........................................................................................................................

........................................................................................................................................

ii) Sajili ................................................................................................................................

........................................................................................................................................

iii) Lahaja ................................................................................................................................

........................................................................................................................................

iv) Uchanganyaji msimbo/lugha ..................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

v) Kaida za lugha ........................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

b) Taja sifa tano bainifu za sajili ya usafiri wa umma. (alama 5)

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................



**JINA**______________________________ **NAMBARI YAKO**____________________

**SHULE** ______________________________ **SAHIHI YA MTAHINIWA** ______________

**TAREHE** ____________________________

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**Julai/Agosti 2015**
**Muda: Saa 2 ½**

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA NAROK KUSINI

## CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA UPILI KENYA

## KISWAHILI

## KARATASI YA 2

## LUGHA

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

b) Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

c) Jibu maswali yote, andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa.

**Kwa matumizi ya mtanihi pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| A | 15 | |
| B | 15 | |
| C | 40 | |
| D | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Fungua Ukurasa**

**SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma makala haya kisha ujibu maswali.***

Bwire na Nabwire ni mayatima waliozaliwa mapacha. Upacha huu uliwafanya kupendana kuliko ulimi na mate. Kila wakati walishirikiana katika kila jambo walilofanya. Watoto hawa walilelewa na nyanya yao baada ya kifo cha baba yao kilichosababishwa na ajali mbaya ya barabara. Mama yao alifuata njia hiyo kutokana na mshtuko wa moyo alipopokea habari kuwa mpenziwe ameaga dunia. Wakati mauti yalipobisha hodi kwenye milango ya nyumba hiyo , Bwire alikuwa na miaka mitano.

Bibi yao alishika hatamu ya kulea. Wahenga walisema kuzaa si kazi, kazi ni kulea. Nyanya huyo mwingi wa miaka alikuwa mwingi wa utajiri wa moyo. Aliwahudumia wajukuu wake kwa moyo wa imani na upendo. Alihakikisha kuwa kila uchao watoto hawa wamekula, wakasoma na kuvaa kulingana na uwezo wake. Hakuna hata siku moja vijana hawa waliwahi kulalamika kwa sababu ya kukosa.

Katika darasa vijana hawa walikuwa wembe. Hawakutaka kucheza ngoma goya. Walifahamu kuwa mchelea mwana kulia hulia yeye. Nayo ajizi ni nyumba ya njaa. Kila wakati walibukua mabuku yao bila hati hati wala tafrani. Matopa kwa matopa waliyasoma kwa lengo na nia ya kujikwamua kutoka lindi la umaskini ambalo lilikuwa limewameza. Hata nyanya yao alikuwa mjane aliyegeuka kuwa mfaruku. Kutokana na bidii zao masomoni na kutokubali kushawishika na vishawishi vya dunia, Bwire na Nabwire waliibuka washindi katika shule yao. Kauntini,hakuna hata mmoja aliyewaona. Walikuwa wamefuatana unyounyo kama siafu. Taswira ya kuwa maskini haikuwa katika akili zao kamwe.

Shule za sekondari waliingia kwa mahanjamu kedekede. Wafadhili walijitokeza kuwafaa vijana hao vikote. Kila wahedi alitaka kuhusana nao katika hali moja au nyingine. Mahitaji ya shule yalinunuliwa na mama Tumaini. Karo ililipwa na hazina ya ufadhili ya maeneo bunge. Gavana alijitolea kuwafaa na la mvua kwa jua. Kidat cha kwanza kiliwalaki kwa mikono miwili. Kila mwalimu alitaka kuhusiana na vijana hawa. Bwire alijiunga na shule ya maghulamu ya Friends Kamusinga naye Nabwire alijiunga na shule ya mabanati ya Lugulu. Kumbe huo ndio ulikuwa mwanzo wa ngoma ya masomo.

Muhula wa kwanza ulitosha kwa wanafunzi hawa kudhihirisha kuwa wao ni mabingwa katika Kaunti ya Busia. Wembe ulikuwa ule ule. Kila wakati, mapacha hawa walikuwa washindi. Hakuna hata siku moja walikuwa washinde. Kila somo walikuwa warajusi. Kila mwalimu alibaki kinywa wazi. Vipi mwanafunzi awe gwiji katika masomo yote? Haya yalikuwa maswali yasiyokuwa na majibu. Majibu yalikuwa wazi. Sijui vipi walitaka kuandikia mate na wino upo.

Ajabu iliyowashangaza walimu shuleni ni kwamba kila mmoja anapokuwa mgonjwa katika shule yake, huko kwingine mambo ni yayo hayo. Kulingana na mtaalamu wa saikolojia, watoto hawa walikuwa na hisia fulani ambazo ziliwaunganisha pamoja licha ya mmoja kuwa mvulana na mwengine kuwa msichana. Mtaalamu huyo alisema kuwa hali hiyo huwaathiri wale ambao ni wa jinsia moja.
Baada ya miaka minne kidatoni, ulifika wakati wa kuchukua kapu kuvuna ulichopanda. Mtihani wa kidato cha nne ulikaribia kutangazwa kama desturi ya kwetu. Bwire na Nabwire ndiyo majina yaliyotajwa ya kwanza kwenye orodha iliyosomwa na waziri wa elimu. Kila mmoja alitaka taaluma ya uhandisi wa ngamizi. Naam, wasemao husema: mchanikia mpinini hafi kwa njaa naye mtafutaji hachoki na akichoka keshapata.

Chuo kikuu waliingia kusomea taaluma moja. Kila mmoja alitaka taaluma ya uhandisi wa ngamizi. Chuo kikuu cha Nairobi kiliwakongowea. Kila shirika lilitaka kuwaajiri vijana hawa kabla ya kumaliza masomo yao. Walijifunga vibwebwe katika masomo yao wakimaizi kuwa mustakabali wao umo ndani ya masomo yao ambayo ni elimu. Hakuna kingine kitakachokuvusha ng'ambo nyingine ya mto wa maisha kama si elimu. Siku moja Bwire alimtazama Nabwire kwa macho maangavu kabla ya kumpiga pambaja. Katika kukumbatiana huko, Bwire alimnong'onnezea Nabwire kwa sauti ya chini kuwa , 'uyatima si kisiki cha ufanisi'.



d) Fuata maagizo kugeuza sentensi hii. (alama 2)

Je, hukuwahi kupita mtihani wowote? ( wakati uliopita hali yakinishi)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

e) i) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

ii) Ainisha vishazi katika sentensi hii. (alama 2)

Mwanafunzi aliyesoma kwa bidii amepata mfadhili.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

f) Andika maana mbili za neno: panda. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

g) Changanua sentensi hii kwa jedwali. (alama 2)

Wanafunzi wanaandika ilhali walimu wanasoma.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

h) Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Babu alimjengea nyanya nyumba kwa mabati

..........................................................................................................................

I) Tunga sentensi moja kubainisha maana za vitate hivi : tua na toa. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

j) Onyesha matumizi mawili ya kibainishi katika sentensi mbili tofauti. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

k) Kanusha sentensi hii. (alama 1)

Karibu na ziwa hilo kulikuwa na mbuga ya wanyama.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

l) Andika kwa wingi. (al.2)

Yeyote anaweza kunisomea aya hiyo.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

m) Ainisha kiunganishi katika sentensi hii. (al.2)

John aliomba mkopo au ruzuku?

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

**Nakala safi**

..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................

**C: MATUMIZI YA LUGHA** (al.40)

a) i) Tofautisha konsonanti na irabu. (alama 2)

..................................................................................................
..................................................................................................

ii) Taja sifa mbili za sauti /j/. (alama 1)

..................................................................................................
..................................................................................................

b) Ainisha vitenzi katika sentensi hii. (alama 3)

Mwalimu alikuwa angali anafundisha Kiswahili.

..................................................................................................
..................................................................................................

c) Geuza sentensi hii katika kauli ya kutendea. (alama 2)

Nilizomewa na wazee hao kupita kiasi.

..................................................................................................
..................................................................................................



Maswali

1. Ipe taarifa uliyoisoma anwani mwafaka. (alama 1)

..................................................................................................

2. Taja sifa mbili zilizowatofautisha mapacha hawa na wenzao shuleni. (alama 2)

..................................................................................................
..................................................................................................

3. Mwandishi ametumia mbinu kadha za lugha katika makala. Taja mbili na kuzitolea mifano. (alama 4)

..................................................................................................
..................................................................................................

4. Huku ukirejelea makala, dhibitisha ukweli wa msemo, 'uyatima si kisiki cha ufanisi'. (alama 3)

..................................................................................................
..................................................................................................
..................................................................................................

5. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika makala. (alama 3)

i) nyanya huyo mwingi wa miaka

..................................................................................................
..................................................................................................

ii) kuchukua kapu kuvuna ulichopanda

..................................................................................................
..................................................................................................

iii) chuo kikuu cha Nairobi kiliwakongowea

..................................................................................................
..................................................................................................

6. Mapacha hawa walipoingia shuleni, ni nini kilichobainika wazi? Kwa nini? (alama 2)

..................................................................................................
..................................................................................................

**B. UFUPISHO** (al.15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali.

Ufisadi ni janga linaloleta maangamizi kwa watu wanaoishi katika nchi. Ufisadi hujenga mipaka kati ya wananchi. Ufisadi huleta mipaka mikubwa isiyobomolewa kati ya walalahai na walalahoi. Ufisadi huhujumu haki za wana wa taifa. Ufisadi huzima haki kwa yule mnyonge. Ama tuseme mnyonge kupata ni tajiri kupenda. Hilo ndilo neno la pekee lililotisha, litakalotisha na hutisha maendeleo ya nchi. Neno ambalo kila mmoja husema limemnyima uwezo wa kufikia kiwango chake cha maisha aliyotarajia kuishi. Neno lenye silabi nne husababisha maangamizi ya taifa na kusambaratisha uchumi wa nchi hata kama ni tajiri kiwango gani. Mara nyingi neno hili huzua mapinduzi hasa katika bara la Afrika.

Neno hili limegawa mataifa mengi duniani katika misingi ya ukabila. Neno hili limewafanya maskini kusalia maskini na hata kile kidogo walicho nacho kuchukuliwa na wao huku wakiendelea kuwa tajiri. Kila wakati kila mtu analalamika kuwa hakutendewa haki kwa sababu moja au nyingine. Watu wengi wamepoteza maisha yao kwa sababu ya shilingi hamsini. Vyombo vya dola pia vimejiingiza katika jinamizi hili ambalo linatuguguna na kupulizia kama panya. Kila mmoja amesahau kuwa bandu bandu huishia gogo.

Madereva barabarani wanaendesha magari kwa kasi bila kujali usalama wao na wa abiria wao. Mguu wake ukikanyaga kichapuzi haubanduki. Utingo nao hupiga debe kumwamrisha dereva kushika usukani salama. Daladala barabarani huyumba huku na kule kwa sababu ya kutodhibitika vilivyo. Polisi wakiwaona wanapunguza mwendo wakiwa na jani mkononi kumsalimia. Gari lenyewe halikaguliwi wala halina hata bima wala kidhibitimwendo. Baada ya tukio la kifo utasikia abiria waliosalimika na kunusurika kwa tundu la sindano wakisema eti dereva alikuwa akiendesha gari kwa kasi. Walikuwa wapi kumkanya? Umanjunju tu na domo kaya.

Tazama kule vijijini na mijini jinsi watu wanavyoaga dunia kama kuku walioshikwa na kideri. Wengine wanasalia vipofu kwa sababu ya unywaji wa pombe haramu. Kuna pombe halali na haramu? Cha halali ni kipi na cha haramu ni kipi? Hao wagema wanatumia dawa za kuhifadhi maiti kutengenezea pombe. Kemikali hizo wao huzipata wapi? Je, kuna viwanda hapa nchini ambavyo vimehalalishwa kuuza dawa hizo kwa mtu yeyote au wao hupitisha mlango wa nyuma? Ajabu ni kwamba hata polisi wakiwashika, kesho wameachiliwa huru kwa visingizio vya kutokuwa na ushahidi. Ushahidi gani mnataka kama dawa zenyewe mlizipata?

Tumeingiwa na ulafi wa kutaka utajiri wa haraka. Tumesahau kuwa haraka haraka haina baraka. Hata zahanatini na hospitalini hakuna dawa. Ajabu utasikia muuguzi au tabibu akikuelekeza katika duka fulani la kununua dawa. Ukichunguza kwa makini, utagundua kuwa duka hilo ni lake. Dawa zinazouzwa hapo zilitolewa katika hospitali ya serikali. Hospitali zenyewe zimegawika katika makundi mawili au matatu. Kuna za walalahai, walalaheri na za walalahoi. Gharama ya matibabu ni tofauti. Mbona mambo haya hayatufikii baada ya kupata uhuru? Ndio nakubali kuwa nilizaliwa baada ya uhuru kupatikana. Lakini nasikia palikuwepo na hospitali za wazungu na za waafrika, shule za wazungu na za waafrika, barabara za wazungu na za waafrika. Au baada ya mzungu kwenda kwao walibaki wazungu weusi ambao sasa wanatumia hizo hospitali zilizokuwa za wazungu? Niambieni ili nipate kujua.

MASWALI

a) Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno 60. (al. 7) 1 utiririko.

**Nakala chafu**



**Nakala safi**

b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno 70-80. (al.8) 1 utiririko.

**Nakala chafu**